# DOYEN PUBLISHERS
## KENYA JUNIOR SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT
## MTIHANI WA MUHULA WA 1 2025
## GREDI YA 9 – KISWAHILI
*(Kartasi ya 1 - Kiswahili Lugha)*

**Muda: Saa 1 dakika 40**

JINA: ______________________________________________

SHULE: _____________________________________________

KITENGO: ______________________ TAREHE: ________________________

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

a) Andika jina lako, shule, kitengo na tarehe katika sehemu zilizo hapo juu.
b) Karatasi hii ina maswali 50 ya uchaguzi wengi. Jibu MASWALI YOTE katika kijitabu hiki cha maswali.
c) Majibu yote lazima yatolewe kulingana na miongozo ya maswali.
d) Kwa kila swali kutoka 1 hadi 50, kuna majibu manne. Majibu haya yameandikwa A, B, C na D. Kila wakati, moja tu kati ya majibu manne ndio sahihi. Chagua jibu sahihi na uandike kwenye jedwali lililo chini.
e) Fanya kazi zote za kujaribu kwenye karatasi ya maswali.

**JEDWALI LA MAJIBU**

| 1. | 2. | 3. | 4. | 5. | 6. | 7. | 8. | 9. | 10. | 11. | 12. | 13. | 14. | 15. | 16. | 17. | 18. | 19. | 20. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |

| 21. | 22. | 23. | 24. | 25. | 26. | 27. | 28. | 29. | 30. | 31. | 32. | 33. | 34. | 35. | 36. | 37. | 38. | 39. | 40. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |

| 41. | 42. | 43. | 44. | 45. | 46. | 47. | 48. | 49. | 50 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

**ALAMA ZA MWANAFUNZI**

| | |
|---|---|
| **Kutoka kwa 50** | |

***Karatasi hii ina kurasa 7 zilizopigwa chapa. Watahiniwa wanapaswa kukagua karatasi hii ili kuhakikisha kuwa kurasa zote zimepigwa chapa kama ilivyosemwa na hakuna maswali yanayokosekana.***

***Soma kifungu kilichofuata kisha jibu swali la 1 hadi 5***

Muda ulio mbele ya mtu ni kama jangwa lisilo na kifani. Katika jangwa hilo, kila mmoja huenda akajikuta akimtafuta mungu wake mwenyewe. Na katika safari hiyo, hujua kuwa kila hatua ni yenye umuhimu na hakuna muda wa kurudi nyuma.

Hali hii humfundisha mtu kuwa nguvu alizonazo sasa ni muhimu zaidi kuliko alichokuwa nacho zamani. Kama vile mvuvi anavyohitaji samaki kwa ufanisi, ndivyo ilivyo kwa mtu katika maisha yake. Usikate tamaa kwa kushindwa, bali jitahidi na utavuna matunda ya juhudi zako.

1. Eleza maana ya methali inayosema "**Muda ulio mbele ya mtu ni kama jangwa lisilo na kifani**."
   A. Muda unaofuatia hauwezi kuonekana au kudhibitiwa.
   B. Muda wa nyuma hauwezi kurejeshwa.
   C. Muda mbele unaweza kuwa na mafanikio makubwa.
   D. Muda ni rahisi kuuelewa na kuufanya.

2. Fafanua maana ya kifungu hicho kwa kumtumia mvuvi kama mfano.
   A. Mvuvi anahitaji kazi nyingi ili kuvua samaki.
   B. Mvuvi anavua samaki bila juhudi yoyote.
   C. Mvuvi anategemea samaki kuishi.
   D. Mvuvi anavua kwa kutumia mitindo tofauti.

3. Ni sentensi ipi imetumika kueleza maana ya "**muda wa kurudi nyuma**."
   A. Hatuwezi kubadilisha kilichopita, ni vyema kuzingatia sasa.
   B. Muda wa kurudi nyuma ni muhimu zaidi kuliko sasa.
   C. Muda wa nyuma ni bora kuliko mbele.
   D. Kurudi nyuma kuna manufaa zaidi kuliko kwenda mbele.

4. Ni jambo lipi tunalojifunza katika kifungu hiki?
   A. Kujua kuwa hakuna jambo linalowezekana.
   B. Kukubaliana na changamoto na kuendelea mbele.
   C. Kutoa juhudi kidogo na kuachia matokeo.
   D. Kusahau kuhusu malengo yako.

5. Je, kifungu hiki kinatoa wito gani kwa msomi?
   A. Aache kujitahidi na akubali kushindwa.
   B. Akubali kuwa kila hatua ni muhimu na ajitahidi.
   C. Afanye maamuzi bila kujali juhudi zake.
   D. Afanye kazi kwa haraka na asijali matokeo.

***Soma kifungu kilichofuata kisha jibu swali la 6 hadi 10***

Walikuwa wakichangamka kwa furaha na shauku kubwa. Ingawa majukumu yao yalikuwa magumu, walijivunia kazi zao kwa sababu walijua kuwa mchango wao ulisaidia kuboresha maisha ya wengine. Wakati mwingine, kilio cha juhudi na machungu kilikuwa hakiwezi kuepukika, lakini walijua kuwa hawakuwa peke yao.

Jamii yao iliwasaidia na kuwapa nguvu za kuendelea. Hali hiyo iliwafanya waendelee kupambana licha ya changamoto zilizozunguka maisha yao. Walijua kuwa kushinda kwao kusingekuwa rahisi, lakini walikuwa na matumaini na imani katika juhudi zao.

6. Eleza maana ya neno "**shauku kubwa**" katika kifungu hiki.
   A. Kupata matokeo bora bila juhudi.
   B. Kujivunia na kufurahia kila hatua ya kazi.
   C. Kuelimika na kujiandaa kwa maisha ya baadaye.
   D. Kushindwa kutimiza malengo kwa urahisi.

7. Nit mtindo wa uandishi uliotumika katika kifungu hiki.
   A. Matumizi ya mifano inayohusisha watu wengi.
   B. Matumizi ya utani na kejeli.
   C. Matumizi ya mifano ya watu binafsi na hali halisi.
   D. Matumizi ya mabishano na kutokuafikiana.

8. Kwa mujibu wa kifungu hiki, ni kipi kinachowapa watu nguvu za kuendelea?
   A. Ujumbe wa kutokukata tamaa.
   B. Upendo wa familia zao.
   C. Jamii inayowasaidia na kuwa na matumaini.
   D. Hali ya upweke.

9. Toa mfano wa hali ya maisha inayohusiana na kifungu hiki.
   A. Mtu anayeishi bila malengo.
   B. Mtu anayejitahidi kufikia malengo licha ya changamoto.
   C. Mtu ambaye hapendi kazi.
   D. Mtu anayeishi kwa kutegemea wengine.

10. Fafanua maana ya neno "**kilio**" katika kifungu hiki.
   A. Furaha na shauku.
   B. Machungu na shida.
   C. Ujasiri na matumaini.
   D. Taa na mwangaza.

***Soma kifungu kilichofuata kisha jibu swali la 11 hadi 20***

Bila shaka, umewahi kushiriki katika michezo mbalimbali shuleni au kijijini. Hata hivyo, nikikuuliza kuhusu umuhimu wa michezo hiyo katika maisha yako, huenda ukachukua sekunde moja au mbili kujibu. Kwa nini hali iwe hivyo? Ni kwa sababu upo wakati katika maisha yetu ya utoto na hata ya utu uzima ambapo tunashiriki katika shughuli fulani kabla ya kuipa fikira ifaayo. Wakati mwingine tunajipata tukiuma vidole: tumejiponza kwa uamuzi wetu.

Sijui unajihisi vipi wakati ambapo unashiriki na wenzako katika michezo kama vile kibe au mwajificho. Je, wakati ambapo unajificha nyuma ya mlango wa sebule, mnuna au mlungizi wako anapotafuta kwa udi na uvumba asikupate, unahisi vipi? Si unajihisi kuwa shujaa au bingwa? Je, hili linakupa hamu zaidi ya kutafuta mikakati bora ya kujificha ili nao watafute mbinu bora zaidi za kukutafuta? Je, wakati unawasikiliza kutoka mafichoni wakikuita, "Mweledi, tafadhali jitokeze," si unaingiwa na fahari kwa kuwa mshindi? Hivyo ndivyo tulivyohisi tulipocheza kibe zamani.

Yumkini umewahi kurusha tiara kwenye uwanja wa shule. Huu ni mchezo ambao tuliupenda sana tukiwa watoto. Nakumbuka wakati huo ningesimama katikati ya uwanja mkubwa wa michezo kijijini mwetu. Ningeishika tiara yangu na kuitupa juu, naiamrisha ipae. Tiara ingepaa kwa mbwembwe juu huko mbinguni, ikifika kileleni mwa mbingu jinsi kipungu afanyavyo. Katika hali hii, licha ya kuburudika, ningejihisi kana kwamba naumiliki ulimwengu mzima; nimeweza kuyadhibiti maisha yangu na kukidhibiti chombo chenyewe. Najua pia umewahi kushiriki katika michezo mingine ya watoto kama nilivyofanya. Kumbuka ulivyojifanya wewe ni mama, unawapikia na kuwafumia fulana watoto wako. Kumbuka ulivyoona fahari wenzako walipokuita mama, nawe unawahimiza kuwa na nidhamu; wakati mwingine hata unamwigiza mzazi wako kwa kuwapiga! Najua

nikikuuliza utaniambia kwamba michezo kama hii ilikusaidia kupalilia kipawa chako cha uigizaji. Haitakuwa ajabu ukiniambia kuwa hivi sasa wewe ni mwigizaji mahiri katika shule yako.

Ikiwa ulikulia katika kijiji ambacho familia ziliishi karibu karibu, utakumbuka jinsi aghalabu mlivyokusanyika kila mchana na hata jioni kupitisha muda. Sijui kama uliwahi kushiriki katika vikao vya kushindana utamkaji wa vitanza ndimi, kutega na kutegua vitendawili, na hata kutambiana hadithi. Ni dhahiri kwamba, licha ya vikao hivi kuwaleta pamoja kama wanakijiji, viliwachangamsha na kunoa bongo zenu. Najua utaniambia kuwa vikao hivi viliibua ucheshi mkubwa. Kumbuka namna ulivyomcheka mwenzako wakati alipotamka vibaya, naye akakukumbusha jinsi ulivyoshindwa kuruka kamba katika mchezo wa kuruka kamba!

Ni wazi kwamba michezo ina manufaa makubwa kwako. Ukipigia darubini maisha yako ya utotoni, utakumbuka ule mchezo wa kuketi katika duara huku mmoja wenu akikimbia kuzunguka duara hiyo na kumpokeza mmoja wenu zamu yake kukimbia kwa kumpiga kwa kitambaa fulani begani au hata kichwani. Mbio hizi si tofauti na zile wanazoshiriki wakimbiaji hodari nchini. Pamoja na kunyoosha misuli na kupumzisha akili, mbio hizi huimarisha afya ya anayeshiriki. Yeye kila mara hujihisi mwepesi kama unyoya. Chakula anachokula hutumika vyema mwilini, hivyo kukinga dhidi ya kujinenepea ovyo.

Usidhani ni mbio tu ambazo ni muhimu. Ipo michezo mingine kama vile uogeleaji na kandanda. Nakumbuka kijijini fuliogelea na kupiga kachombe kwenye vidimbwi na mabwawa ya kiasili. Siku hizi mmejengewa mabwawa maalumu. Wachezaji wa michezo kama hii hupata umaarufu kitaifa na kimataifa. Hali kadhalika, wachezaji wengi wameweza kujiendeleza kiuchumi kutokana na fedha wanazopata kutoka michezoni. Wengine hujipatia marafiki wa kudumu kupitia michezo hii. Wapo hata waliowahi kufunga ndoa na waja kutoka mataifa mengine!

Ni muhimu kukumbuka kwamba ule wakati ambapo michezo ilihusishwa na watu wasiojiweza kimasomo umetupa kisogo. Ni muhimu kuanza kutambua na kuvitumia vipawa vyetu kwa njia ifaayo. Wale walio na vipawa katika michezo nao watahadhari dhidi ya kuchukua muda wao wote katika mchezo na kuyapuuza masomo. Elimu ndiyo itakayokuwezesha kutumia mtaji unaopata michezoni kwa njia inayokufaidi wewe na jamii yako.

11. Katika aya ya kwanza mwandishi:
    A. Ana hakika kwamba msomaji aliwahi kucheza.
    B. Ana tumaini kwamba msomaji anaweza kucheza.
    C. Anajua kwamba msomaji alichezea shule.
    D. Awaza kuwa msomaji atakuwa mwanamichezo kijijini.

12. Aya ya kwanza inaonyesha hali ya watu:
    A. Kufanya mambo yasiyo na faida kwao.
    B. Kujihusisha na shughuli bila kuwazia maana yake.
    C. Kutotambua lengo la michezo shuleni.
    D. Kutozingatia ubora wa kuepuka majuto.

13. Kulingana na aya ya pili, Kibe:
    A. Humfanya mtu kufahamu jinsi wengine wanavyohepa.
    B. Humpa mtu hamu ya kushirikiana na familia.
    C. Humwezesha mtu kujivunia uwezo wake katika jambo.
    D. Hurahisisha juhudi za kuwatafutia wengine suluhisho.

14. Mwandishi:
    A. Alijasirika zaidi kwa kung'amua kwamba amehusika katika kuiboresha dunia.
    B. Alijiamini zaidi kwa kutambua amechangia katika mafanikio yake.
    C. Alijithamini zaidi kwa kufahamu kufanana kwa uwezo wa tiara na wa kipungu.
    D. Alipumbazika zaidi kwa kufikia mbingu wakiwa watoto.

15. Chagua jibu ambalo si sahihi kulingana na aya ya tatu:
    A. Kufanikiwa katika jambo ni njia ya kujenga tabia.
    B. Mtu anapoiga yafanywayo na wengine huwa na mafanikio mengi shuleni.
    C. Tuyafanyayo tukiwa watoto baadaye huathiri mazoea yetu.
    D. Wanajamii wanaweza kurekebisha tabia hata katika shughuli za kawaida.

16. Kifungu kimeonyesha kwamba, ilikuwach kawaida kwa:
    A. Makundi kuandikiana vitanza ndimi.
    B. Nyumba kuwa karibu na nyingine.
    C. Vikao kukumbushana kuhusu kushindwa.
    D. Watoto kujumuika pamoja katika shughuli.

17. Chagua umuhimu wa michezo kwa mujibu wa aya ya nne:
    A. Huimarisha utamkaji wa sauti, huboresha uwazaji.
    B. Hukuza ushirikiano wa kijamii, huokoa wakati.
    C. Huleta ubunifu, hustawisha utani.
    D. Huliwaza washiriki, huwatumbuiza wanaosimulia hadithi.

18. Kwa mujibu wa kifungu:
    A. Mbio za kuzunguka huifanya akili ya mtu kufikiri vyema.
    B. Michezo husaidia mwili kunufaika kwa lishe upatayo.
    C. Urafiki wa dhati hupatikana baada ya michezo.
    D. Waogeleaji hupata sifa wanapoogelea ng'ambo.

19. Kulingana na aya ya mwisho elimu:
    A. Humpa mtu fursa ya kujua namna ya kupanga wakati ili kuimarisha utendakazi.
    B. Humpa mtu stadi za kutumia alichofanikiwa na kuinua jamii.
    C. Humwezesha mtu kufahamu nafasi aliyo nayo.
    D. Humwezesha mtu kutambua faida ya vipawa.

20. Maana ya umetupa kisogo ni:
    A. Umebadilika.
    B. Umepita.
    C. Umepuuzwa.
    D. Umesahaulika.

***Kifungu kifuatacho kina nafasi 21 hadi 28. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kujaza nafasi.***

Mtu _____**21**_____ lugha huanza kwa kutamka sauti za lugha hiyo. Sauti hizo huambatana _____**22**_____ kuunda silabi. Neno _____**23**_____ kwa idadi maalum ya silabi. Mathalani, neno, 'iliyowambwa' lina silabi _____**24**_____. Mtumiaji wa lugha pia hujifunza viambishi vya aina mbalimbali. Kwa mfano, 'ku' katika, 'alikutarajia ufike' inaonyesha _____**25**_____. Maneno _____**26**_____ ni muhimu katika kuwasiliana. Kwa mfano, neno 'hewala' ambalo ni _____**27**_____ huonyesha _____**28**_____.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 21. | analojifunza | anayojifunza | anaojifunza | anapojifunza |
| 22. | ili | maadamu | lao | minajili |
| 23. | hujengewa | hujenga | hujengwa | hujengea |
| 24. | 4 | 5 | 6 | 3 |
| 25. | kitenzi | wakati | mahali | nafsi |
| 26. | nao | nazo | nayo | nako |
| 27. | kielezi | kihisishi | kiunganishi | kivumishi |
| 28. | kukubaliana na jambo | kuajabia kitu unachoona | kuomba kitu kisimuumize mtu | kueleza jinsi jambo litendekavyo |

***Kutoka swali la 29 hadi la 50 chagua jibu sahihi.***

29. Maneno haya hufuatana vipi katika kamusi?
    (i) shwari
    (ii) sinzia
    (iii) sentensi
    (iv) staha
    A. iii, ii, i, iv
    B. ii, iii, i, iv
    C. ii, i, iii, iv
    D. iii, i, ii, iv

30. Ni kipi kisicho kihusishi vya wakati?
    A. tangu
    B. hadi
    C. kwenye
    D. kisha

31. Chagua sentensi iliyoakifishwa ipasavyo.
    A. Mzee alikuwa na bidhaa zifuatazo: kabati, meza, viti, na rafu.
    B. Kadi, hujamaliza kazi hiyo nyepesi, hivyo!
    C. Wanafunzi wake - Wale waliopata alama za juu zaidi - wanatuzwa leo.
    D. Mkulima alipanda nafaka* yaani (wimbi na mlama)

32. Wingi wa sentensi, ‘**Karani yule alimpelekea mkurugenzi waraka huo**’, ni:
    A. Karani yule aliwapekelea wakurugenzi waraka huo.
    B. Makarani wale waliwapekelea wakurugenzi nyaraka hizo.
    C. Makarani wale walimpelekea mkurugenzi waraka huo.
    D. Karani yule alimpelekea mkurugenzi nyaraka hizo.

33. Chagua kauli ya kutendewa ya sentensi ifuatayo: "Menza alikwenda kwa Tumaini akakata kuni."
    A. Tumaini alikatiwa kuni na Menza.
    B. Tumaini alikatiwa kuni kwa Menza.
    C. Menza alikata kuni kwa Tumaini.
    D. Tumaini na menza walikatiana kuni.

34. Neno lipi lenye sauti mwambatano?
    A. mvua
    B. liwa
    C. kunja
    D. wayo

35. Chagua jibu lenye maelezo sahihi.
    A. Kefule! - ni tamko linalotumiwa kuonyesha kuudhika.
    B. Hewala! - hutumiwa baada ya kuupata ushindi fulani.
    C. Simile! - ni tamko linalotolewa baada ya kumruhusu mtu kupita.
    D. Makiwa! - hutumiwa ili kumpa pole mtu aliyepoteza bidhaa zake.

36. Bainisha sentensi isiyo na -ki- ya masharti.
    A. Tukitumia teknolojia tutaweza kufika mbali.
    B. Kitabu hiki ni changu.
    C. Tukipanda miti mingi, viwango vya mvua vitaongezeka.
    D. Mkulima huyu akitumia mbolea ifaayo, atapata mazao mengi.

37. Kukanusha kwa ‘**Simba ambao wamejeruhiwa wametibiwa**’, ni:
    A. Simba ambao wamejeruhiwa hawatatibiwa.
    B. Simba ambao hawakujeruhiwa hawatatibiwa.
    C. Simba ambao wamejeruhiwa hawajatibiwa.
    D. Simba ambao hawajajeruhiwa hawajatibiwa.

38. Chagua jibu lenye maelezo sahihi.
    A. Kisasi ni tendo la kumlipizia mtu kosa alilotenda, na kizazi ni watu wanaoishi katika jamii moja.
    B. Zabuni ni zawadi anayopata mtu mashindanoni, na sabuni ni madini yanayotumiwa kusafisha nguo.
    C. Kudanda ni kuruka ili kukishika kitu, ilhali...
    D. Kushtaki ni kumkataa mtu.

39. Ujanja ni kwa sungura ilhali _______________ ni kwa kabuzi.
    A. kawaida
    B. ghafla
    C. utulivu
    D. msiri

40. Ni jibu lipi lisilolingana na mengine?
    A. alamsiki - binuru
    B. shikamoo - marahaba
    C. masalkheri - sabalkheri
    D. hodi - karibu

41. Chagua sentensi iliyounganisha sentensi zifuatazo ipasavyo:
Nyumba ilikuwa kubwa. Nyumba haikuwatoshea wageni wote.
   A. Nyumba ilikuwa kubwa angalau haikuwatoshea wageni wote.
   B. Nyumba ilikuwa kubwa madhali haikuwatoshea wageni wote.
   C. Licha ya nyumba kuwa kubwa haikuwatoshea wageni wote.
   D. Nyumba ilikuwa kubwa licha haikuwatoshea wageni wote.

42. Chagua sentensi inayoonyesha hali ya kuagiza.
   A. Angetaka angewaimbia.
   B. Meza tembe mbili mara moja.
   C. Watakaosoma vyema watapita mtihani wao.
   D. Ulileteva hilo.

43. Ni sentensi ipi yenye kiambishi 'ki' cha ngeli pekee?
   A. Mukai alikibeba mgongoni.
   B. Shime alienda kijijini.
   C. Dola anazungumza akitabasamu.
   D. Timau akiija tutafurahi.

44. Chagua jibu lenye maneno yasiyoambatanishwa ipasavyo.
   A. funguo - kicha
   B. nzige - wingu
   C. hindi - bunzi
   D. maji - funda

45. Ni jibu lipi lenye vivumishi pekee?
   A. gumu, upesi, nadra, langu
   B. safi, yote, sana, halafu
   C. nne, kama, mno, bora, pengine, zile, kwao
   D. mrembo, tamu, chungu, jeupe

46. Tambua kiwakilishi kionyeshi katika sentensi hii:
Huyo ni mchezaji maarufu wa mpira wa miguu.
   A. huyo
   B. ni
   C. maarudu
   D. wa

47. Ni neno lipi lisilo na sauti /g/?
   A. gari
   B. ghali
   C. giza
   D. gombea

48. Mjomba ni kwa shangazi ilhali buda ni kwa ___________________
   A. ajuza
   B. ghulamu
   C. shaibu
   D. kigoli

49. Konga ni kuzeeka, konga pia ni _________________
   A. Kutumia mrija kuvuta kinywaji baridi.
   B. Kuleta watu pamoja kwa shughuli fulani.
   C. Kupunguza hamu ya kitu usicho nacho.
   D. Kukubaliana na jambo ambalo wengine wamelijadili.

50. Kauli iliyopigiwa mstari imetumia tamathali gani ya usemi?
Matone makali ya mvua **yaliusalimia** uso wake.
   A. Nahau
   B. Sitiari
   C. Ishara
   D. Tashhisi

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**